JAMHURI YA MUUNANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za simu Shule ya Sekondari Mwenge,

Mkuu wa Shule 026 250 2095/0763 264 024 S.L.P 195,

Makamu Mkuu wa Shule 0717720932/0765840160 **SINGIDA.**

Tarehe ……..

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi……..

S.L.P ……

……..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWENGE

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA MKOANI SINGIDA

MWAKA 2018

- Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018/2019 tahasusi ya ……..

Shule ya Sekondari **Mwenge** ipo Singida mjini kilometa moja na nusu kaskazini kutoka stendi kuu ya mabasi "Misuna Bus terminal." Usafiri kutoka stendi hadi shuleni ni wa **bajaji/ pikipiki**. Nauli ni shilingi elfu mbili **(2,000/=)** kwa bajaji na shilingi elfu moja **(1,000/=)** kwa pikipiki. Usafiri huu unapatikana katika kituo cha mabasi.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **……..** Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……..** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **……..**

- **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**
    - **Sare ya Shule**

- Shule hii ni ya **bweni** na ni ya **wavulana pekee** hivyo sare ya shule hii ni kama ifuatavyo:-
    - Shati mbili nyeupe za tetroni mikono mirefu.
    - Suruali mbili za rangi ya **"jungle green".** Suruali hizi zishonwe **bila** kuwekewa marinda na ziwe na mfuko mmoja wa nyuma usiokuwa

  na zipu wala kifuniko. Pia isiwe ya kubana wala mdomo wa chupa miguuni. Aina ya kitambaa cha suruali ni hiki kilichoambatanishwa hapa chini.

    - Sweta **moja** ya mikono mirefu rangi ya "jungle green" yaani rangi inayofanana na rangi ya kitambaa cha suruali. Sweta hiyo iwe na shingo ya mshono **V** na mikono mirefu.
    - Tai **mbili** zenye mistari **myeupe** na **"jungle green."**
    - Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
    - Soksi jozi mbili nyeupe/nyeusi/ khaki
    - Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi
    - Nguo za kushindia "shamba dress" ni suruali mbili za kitambaa cha khaki zenye mshono kama zile za jungle green na "T.Shirt" yenye kola na vifungo vitatu.

  Muonekano wa sare hizo ni kama ulivyo kwenye kiambasho ukurasa wa sita (06)

    - Mwanafunzi aje na jezi moja ya michezo yaani bukta na "T.Shirt" kwa mchanganuo ufuatao:

  HGL -Jezi nyeusi mistari myeupe

  HGK - Jezi ya rangi ya chungwa mistari myeusi

  HKL - Jezi nyeupe mistari myeusi

  EGM - Jezi ya zambarau mistari myeupe

  CBG - Jezi nyeusi mistari ya njano

  PCB - Jezi nyekundu mistari myeupe

  PCM - Jezi ya blue mistari ya njano

HGE- Jezi rangi ya maruni na mistari myeupe

ANGALIZO: Mwanafunzi **haruhusiwi** kufika shuleni na nguo nyingine yeyote tofauti na hizo alizoagizwa kwenye barua ya maelekezo.

- **Ada na michango ya shule**
  - **Ada ya shule** kwa mwaka ni shilingi **70,000/=** kwa mwanafunzi. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi **35,000/=** kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha za ada **sh 35,000/= au sh 70,000**/=zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na **5081100022** katika Benki ya **NMB.** Jina la akaunti ni Mwenge Secondary School Education Development.
  - **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi kwa kila mwanafunzi ni:**
    - Shilingi **15,000/=** kwa ajili ya ukarabati wa samani
    - Shilingi **6,000/=** kwa ajili ya kitambulisho
    - Shillingi **20,000/=**kwa ajili ya taaluma
    - Shilingi **30,000/=** kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
    - Shilingi **2,000/=** nembo ya shule
    - Shilingi **10,000/=** kwa ajili ya huduma ya kwanza kwa wasio na bima ya afya na shilingi **5,000/=** kwa wenye Bima ya Afya

    (wanafunzi wanashauriwa kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya CHF)

    - Shilingi **5,000/=** kukodisha godoro kwa muhula na yanapatikana shuleni
    - Fedha ya tahadhari shilingi **5,000/=** (Hairudishwi)
    - Shilingi **20,000/=** mitihani ya kujipima mock (Fedha hii italipwa baada ya mwanafunzi kuingia kidato cha sita Julai 2018).

Fedha za michango mbalimbali zilipwe kwenye akaunti ya shule **Na 5081100036 NMB.** Jina la akaunti ni Mwenge Secondary School Self Reliance. Tafadhali zingatia kuweka fedha husika kwenye akaunti husika. Andika jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi kwenye "pay in slips" na kukabidhi kwa muhasibu wa shule.

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

- "Ream" 1 ya karatasi (kwa mwaka)
- "Scientific calculator" kwa watakaosoma sayansi au uchumi
- Mashuka rangi ya "light blue" jozi 1, blanketi 1 na chandarua
- Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
- Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa kila mwanafunzi

VIFAA VYA USAFI KWA TAHASUSI NI KAMA IFUATAVYO:

1. **HGL, EGM, PCB na CBG** - Kwanja, ufagio wa ndani "soft broom" 1, ufagio wa nje (chelewa) 1,"Rubber Squeezer" na "hard broom".

2**. HGK na PCM -** Kwanja, ufagio wa ndani "soft broom" 1, ufagio wa nje (chelewa) 1 na reki yenye mpini wa chuma.

- **HKL na HGE –** Kwanja, ufagio wa ndani "soft broom" 1, ufagio wa nje (chelewa) 1 na jembe

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

- Wizi
- Kutohudhuria masomo kwa siku **90** au zaidi bila taarifa/ utoro.
- Kugoma au kuhamasisha mgomo.
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu mwingine.

- Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
- Kufuga ndevu.
- Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
- Uvutaji wa sigara.
- Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
- Kupata ujauzito au kutoa mimba
- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
- Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- Kukutwa anamiliki au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- Kudharau Bendera ya Taifa.
- Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi
- Makosa mengine ya jinai.

- **VITAMBULISHO NA FOMU MUHIMU**
  - Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga wa hospitali ya Serikali)
  - Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
  - Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

- Picha moja moja na namba za simu za wazazi/walezi na ndugu wanne wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni
- Cheti halisi cha kuzaliwa na nakala yake
- Hati halisi ya matokeo "result slip" ya kidato cha nne na nakala yake.

- Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Mwanafunzi atasajiliwa tu baada ya kutekeleza maagizo haya na kukabidhi fomu zilizojazwa kikamilifu na si vinginevyo.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII

Bonus P. Ndimbo
Mkuu wa Shule

KIAMBATISHO A.

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWENGE
A: SEHEMU YA MWANAFUNZI
MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII

- Mimi ----------ninakubali kujiunga na Shule ya Sekondari Mwenge katika Kidato cha ----------kwa tahasusi ya ----------
- Nikiwa mwanafunzi wa Mwenge Sekondari, ninakubali kwamba:-
    - Nitafika shuleni siku ya kufungua na bila kuchelewa kila muhula
    - Nitatii sheria zote za shule pamoja na kutoshiriki katika ulevi, migomo na migogoro ya aina yeyote.
    - Sitaleta shuleni wala kuvaa mavazi yasiyoruhusiwa na yasiyo ya heshima k.m nguo za kubana, kofia, miwani ya giza, pete za urembo n.k.
    - Nitatumia juhudi na maarifa yote kujiimarisha kitaaluma ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vipindi na kufanya mazoezi na mitihani yote.

Saini ya Mwanafunzi ----------Tarehe ----------

B: SEHEMU YA MZAZI /MLEZI

MZAZI/MLEZI AJAZE SEHEMU HII

- Mimi----------nimekubali mtoto wangu ----------ajiunge na shule ya Sekondari Mwenge kuanzia tarehe----------

Ninaahidi kwamba:

- Nitawasaidia walimu kumlea mwanangu kitaaluma na kitabia. Nitamuonya na kumsisitiza mwanangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri kwa maadili ya kiuanafunzi.
- Nitamkataza kuvaa nguo zisizo za heshima k.m. nguo za kubana, kofia, miwani ya giza n.k
- Nitampatia mtoto wangu nauli ya kuja shuleni na kurudi likizo bila kuchelewa.
- Nitahakikisha anakuja shuleni siku ya kufungua kila muhula bila kuchelewa .
- Anwani yangu ya kudumu

Saini ya Mzazi / Mlezi ---------- Tarehe----------

(Tafadhali njoo na fomu hii unapokuja shuleni ikiwa imejazwa)

KIAMBATANISHO B.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
MWENGE SEKONDARI
FOMU YA MAELEZO BAYANA (PERSONAL PARTICULARS)
KWA AJILI YA USAJILI (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

- Jina kamili la mwanafunzi kama alivyojiandikisha kwenye mtihani wa kidato cha Nne 2016----------
- Jina kamili la Baba /Mlezi ----------
  - Anwani ya Baba/ Mlezi----------
  - Namba ya simu ya Baba/ Mlezi kazini----------

Nyumbani ----------

- Mtaa/ Kijiji ----------Kata----------Tarafa----------

Wilaya----------anakotoka

- Jina la Mama / Mlezi----------
  - Anwani ya Mama /Mlezi----------
  - Namba ya simu ya Mama/Mlezi----------

Nyumbani ----------

- Mtaa/ Kijiji----------Kata----------Tarafa----------

Wilaya ----------anakotoka

- Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi ----------
- Mahali alipozaliwa ----------Mkoa----------

Wilaya ----------Kijiji/Mtaa----------

- Kazi ya Baba/Mlezi----------
- Kazi ya Mama/ Mlezi----------
- Je mwanafunzi anacho kilema chochote----------
- Taja ndugu wanne ambao wanaweza kutoa msaada au kumtembelea mwanao

No.	JINA KAMILI	KAZI	UHUSIANO	SIMU

TAREHE----------SAHIHI YA MZAZI/MLEZI----------

KIAMBATANISHO C.

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

TO: The Medical Officer From: ----------
---------- ----------
---------- ----------
---------- ----------

Mr.----------

(Name in full)

Please examine the above named as to his physical and mental fitness for a full- time Advanced level of Secondary Education studies The examination should include the following ineligible in case of a defect.

- (a) Eyesight

(b)Hearing
(c)Speech
(d)Limbs
(e)Vuneral Diseases
(f)Leprosy
(g)Epilepsy

- Neuroses
- Other serious diseases

Date:----------Signature----------

PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by a Government Officer)

I have examined the above – named and consider that he/ she is physically fit / unfit and mentally fit/ unfit for a full – time Advanced Level of Secondary Education Studies.

- (a) Eyesight----------

(b)Hearing ----------
(c)Speech----------
(d)Limbs----------
(e)Vuneral Diseases----------
(f)Leprosy----------
(g)Epilepsy----------

- Neuroses----------
- Other serious diseases ----------

Date:----------Signature----------

Station:----------Designation:----------